Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam

# Jarida la SAUTI YA JIJI

Toleo maalum namb. / Dcc/ 016

DAR ES SALAAM

## NANENANE 2023

## WAZIRI PINDA APONGEZA TEKNOLOJIA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI JIJI LA DSM



Waziri Mkuu Mstaafu Mhe Mizengo Kayanza Pinda leo tarehe 1 Agosti, 2023 ametembelea Banda la Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam katika Maonesho ya nane nane kanda ya Mashariki yanayojumuisha Mikoa minne ya Tanga, Pwani,Morogoro na Dar es Salaam yanayofanyika mkoani Morogoro katika Viwanja vya Mwl. Julius Kambarage Nyerere kuanzia tarehe 1-8 Agusti, 2023.
Akiwa ndiye Mgeni rasmi wa ufunguzi wa maonesho hayo , Mhe Pinda ameridhishwa na teknolojia mbalimbali za Kilimo, Mifugo na Uvuvi nalizooneshwa katika banda la Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na kulipongeza Jiji la Dar es salaam kwa maandalizi mazuri yenye ubunifu mkubwa wa teknolojia hizo.

**Habari zaiaidi uk 01**

## JIJI LA DAR ES SALAAM MSHINDI WA KWANZA MAONESHO YA NANENANE 2023 - MOROGORO





## DC MPOGOLO ATANGAZA NEEMA KWA WAJASIRIAMALI ILALA




# Jiji la Dar es Salaam lapongezwa Maonesho ya Nanenane

Waziri Mkuu Mstaafu Mhe Mizengo Kayanza Pinda leo tarehe 1 Agosti, 2023 ametembelea Banda la Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam katika Maonesho ya nane nane kanda ya Mashariki yanayojumuisha Mikoa minne ya Tanga, Pwani,Morogoro na Dar es Salaam yanayofanyika mkoani Morogoro katika Viwanja vya Mwl. Julius Kambarage Nyerere kuanzia tarehe 1-8 Agusti, 2023.
Akiwa ndiye Mgeni rasmi wa ufunguzi wa maonesho hayo , Mhe Pinda ameridhishwa na teknolojia mbalimbali za Kilimo, Mifugo na Uvuvi nalizooneshwa katika banda la Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na kulipongeza Jiji la Dar es salaam kwa maandalizi mazuri yenye ubunifu mkubwa wa teknolojia hizo.

Katika banda hilo Mhe Pinda ameweza kuona Teknolojia mbalimbali ikiwemo Kilimo cha mbogamboga kwa kutumia Kitalunyumba,utengenezaji wa bustani za nyumbani ( home garden ), teknolojia ya uongezaji wa thamani kwenye mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi, kilimo cha uyoga na mapishi mbalimbali ya uyoga, Ufugaji wa samaki kwenye Mabwawa , Kilimo bila kutumia udongo, Ututoleshaji wa Vifaranga vya Samaki, ufugaji wa kuku , mbwa , ngombe wa maziwa pamoja na kutembelea wajasiriamali
Aidha Mhe Pinda pia amepongeza Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam kwa kuanzisha maabara maalum ya upimaji wa afya ya udongo ambayo hutumika kufundisha wakulima teknolojia mbali mbali za kilimo iloyopo Kinyamwezi katika kata Pugu.

Akitoa shukrani kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Ilala Mhe Hashim Komba ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Ubungo amesema kuwa “kwa niaba ya Mhe Edward Mpogolo tunakushukuru sana Mhe Waziri mkuu mstaafu kwa kutembelea banda letu la Halmashauri ya Jiji , Wilaya yetu itaendelea kuwezesha vijana na wanawake ili kuongeza tija kwenye shughuli za kiuchumi wanazofanya”

Aidha Mkuu wa Divisheni ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Ushirika Ndugu Majaliwa Andrea kwa niaba ya Mkurugenzi wa Jiji ameeleza kuwa Halmashauri itaendelea kutekeleza sera za Kilimo, mifugo na uvuvi ikiwa ni pamoja na kutenga Asilimi kumi ya mapato ya ndani ya Halmashauri kuwawezesha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kiuchumi.





# DC EDWARD MPOGOLO ATANGAZA NEEMA KWA WAJASIRIAMALI ILALA

Wajasiriamali wanaojiuhusisha na Biashara mbalimbali katika Jiji la Dar es Salaam wametakiwa kujitokeza kwa wingi kushiriki maonesho maamlum ya biashara na shughuli wanazofanya yanayotarajiwa kufanyika katika viwanja vya mnazi mmoja yenye lengo la kutangaza biashara zao ili kuwainua kiuchumi kupitia kukuza Masoko ya bidhaa zao.

Wito huo umetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Ilala Mhe Edward Mpogolo alipotembelea banda la Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwenye maonesho ya Kilimo maarufu kama nanenane kanda ya Mashariki yanayofanyika katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere Mkoani Morogoro.

“Nawapongeza kwa maandalizi mazuri sana ya kuonesha na kueleimisha watu juu ya Teknolojia za Kisasa za Kilimo , Mifugo na Uvuvi Lakini kama wilaya mara baada ya nanenane mpango wetu ni kufanya Maonesho maalum katika viwanja vya Mnazi Mmoja kwa ajili ya Wajasiriamali wa Jiji la Dar es Salaam kutangaza Biashara zao kwa siku saba ili waongeze masoko ya bidhaa zao kwakua maonesho haya ya nanenane hua yafanyika mara moja tu kwa mwaka hivyo muda hautoshi kwa wajasiriamali wetu kujitangaza zaidi ndio maana tumeona iko haja ya kufanya maonesho ya Wajasiriamali “ alisema mhe Mpogolo

Vile vile Mkuu huyo amezipongeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamojana wizara ya Kilimo kwa kufikiria kaulimbiu ambayo inahamasisha Vijana na Wanawake kuongeza nguvu ya Uzalishaji ili kutimiza azma ya Mhe rais Dkt Samia Suluhu Hassan ya kutaka Tanzania kujitosheleza kwa Chakula pamoja na Kuuza nje ya Nchi.

Maonesho ya Nanenane Kanda ya Mashariki yanashirikisha Mikoa mine ambayo ni Dar es salaam , Tanga, Morogoro na Pwani na hufanyika kila Mwaka ifikapo mwezi agosti na kilele chake huwa ni tarehe nane mwezi Agosti.



## Habari Picha

# ZIARA YA MKUU WA WILAYA KATIKA BANDA LA JIJI LA DSM MAONESHO YA NANENANE 2023 - MOROGORO



Mkuu wa Wilaya ya Ilala Mhe Edward Mpogolo akizungumza na Mjasiriamali aliyewezeshwa Mkopo wa 10 % na Halmashauri ya Jiji la DSM anayejihusisha na Utengenezaji wa Viatu vya Ngozi



Kilimo cha Nyanya



Kilimo cha Mbogamboga



Teknolojia ya Ufugaji wa Samaki kwenye Bwawa lisilo la Kuchimba




Mkuu wa Wilaya ya Ilala akiuzungumza na Mjasiriamali anayejihusisha na Usindikaji wa Viungo na Mazao mbalimbali ya Kilimo



# KANUNI KUMI (10) ZA KILIMO BORA

## 1.KUCHAGUA ENEO LINALOFAA KWA KILIMO

Kitaalamu shamba linalofaa kwa kilimo ni eneo lenye ardhi yenye rutuba, maji na hali nzuri ya hewa na lisiwe mbali na soko la mazao yatokayo shambani.

Vilevile liwe na historia ya kutokuwa na magonjwa mengi ya mimea na wadudu waharibifu.Kuwepo na miundombinu kama vile barabara na mawasiliano.

## 2. KUTAYARISHA SHAMBA MAPEMA

Utayarishaji wa shamba ni zoezi zima la kulima shamba, kuliweka safi kwa ajili ya kilimo cha msimu huo. Husaidia uboreshaji wa mazao katika msimu unaofuata, mkulima anaweza kuyatumia masalia ya mazao ya msimu uliopita shambani kwa kuchanganya na udongo na kuwa chanzo cha mbolea hali ambayo hurutubisha udongo na kuulainisha.

Zoezi hili likifanyika husaidia kuharakisha hewa kupenya katika udongo ambayo ni muhimu kwa wadudu mbalimbali waishio ardhini kurutubisha udongo na kurahisisha mizizi ya zao husika kupenya kirahisi kutafuta virutubisho na mbegu kuota kirahisi.

## 3. KUCHAGUA MBEGU BORA

kustahamili ukame, magonjwa na wadudu kwa kutumia mbegu zenye ubora wa
namna hiyo kutatupa ufanisi na uhakika wa kupata mavuno mengi zaidi.

## 4. KUPANDA MAPEMA NA KWA NAFASI

Husaidia mimea iliyomo shambani kutumia vyema virutubisho mbalimbali vilivyomo kwenye udongo na pia kusaidia mmea kusharabu mwanga wa jua na hivyo kuweza kujitengenezea chakula ambacho ni muhimu kwa makuzi ya mimea na hivyo kutupatia mavuno ya kutosha.

## 5. KUPALILIA MAPEMA

Kupalili ni kitendo cha kuondoa magugu ambayo yataleta madhara kwenye zao husika na pia kuondoa zao ambalo halikukusudiwa katika zao lililopandwa. Kupalilia kuna faida nyingi kwa mazao kama vile kulainisha udongo na kurahisisha mbegu kumea vizuri, mizizi kupenya kiurahisi wakati ikisaka virutubisho kwenye udongo kuruhusu hewa kupita kirahisi ambayo ni muhimu kwa uhai wa vijidudu mbalimbali vinavyoishi ardhini ambavyo vinarutubisha udongo.

## 6.KUPUNGUZA MICHE

Ni kutoa miche iliyozidi kwenye shimo moja na kubakisha mche mmoja wenye afya.
Hii husaidia mimea iliyobakizwa shambani kuweza kutumia virutubisho vilivyomo ardhini kwa kiasi cha kutosha

na hivyo kumea vyema na kuweza kutoa mavuno mengi. Pia inapunguza mlipuko wa magonjwa hasa ya ukungu.

## 7.KUTUMIA MBOLEA ZA KUPANDA, KUKUZIA NA KUZALISHA.

Mbolea za kupandia zinasaidia kuboresha mizizi ya mmea na hivyo kujishika vizuri kwenye ardhi, mbolea za kukuzia zinaipa umbijani mmea na za kuzalishia kuweza kutoa maua na hatimaye kubeba tunda la zao.

Mbolea inasaidia mimea kumea na kukua vyema vile vile hukinga mimea dhidi ya mashambulizi mbalimbali ya magonjwa, wadudu hivyo kuweza kukua vyema na kutoa mazao mengi yenye ubora.

## 8. KUZUIA WADUDU NA MAGONJWA

Hii ni dhana ya kuthibiti wadudu na magonjwa pale tu wanapoonekana kwenye mazao. Husaidia mimea kustawi vyema na kwa haraka na huo ndiyo msingi wa kupata mavuno mengi na bora

## 9. KUVUNA KWA WAKATI NA KUHIFADHI

Inashauriwa kuvuna mazao mara tu yanapokuwa tayari yameshakomaa ili kuzuia kuharibika kwa zao

## 10.KUBADILISHA NA KUTUMIA KILIMO MSETO

Hiki ni kilimo cha mzunguko wa mazao kwa kubadilisha kulima zao la aina moja katika eneo moja muda mrefu na pia
kulima mazao mawili au matatu katika
kulima mazao mawili au matatu katika shamba moja kwa msimu. Inasaidia kurutubisha udongo na pia kupunguza mlipuko wa wadudu na magonjwa shambani

# TEKNOLOJIA YA UHAMILISHAJI KWA NJIA YA CHUPA



Ni teknologia rahisi inayompatia mfugaji ndama bora wa maziwa/nyama

FAIDA ZAKE:

Kupata ng'ombe bora wa maziwa au nyama

Gharama yake ni kidogo ukilinganisha na kufuga dume

Ndama wanakua haraka

Magonjwa ya vizazi ni aghalabu kupata

Ongezeko la mazao (maziwa/nyama)

2. **MAMBO YA KUZINGATIA**:

Ng'ombe wapate lishe bora

Ng'ombe wapewe madini ya kutosha

- Ndama: 40-50gms (viberiti 4-5) kwa siku
- Madume: 50-60gm (viberiti 5-6) kwa siku
- Mitamba: 80gms (viberiti 8) kwa siku
- Majike (ambao wamezaa): siyo chini ya 100gms (yaani zaidi ya viberiti 10) kwa siku kutegemea maziwa anayotoa.

3. UMRI WA KUPANDISHA:

Mitamba ipandishwe kwa mara ya kwanza wafikiapo umri wa miezi 18. Hata hivyo ni vyema kuangalia umbile la mtamba kabla ya kumpandisha.

4. DALILI ZA JOTO:

Kulia mara kwa mara bila sababu yoyote

Kupanda ng'ombe wengine, naye kuruhusu kupandwa.

Kukojoa mara kwa mara

Kutoa ute mwepesi ukeni

Sehemu ya nje ya uke huvimba na kuwa nyekundu

Kupunguza maziwa (kwa wanaokamuliwa)

5. MUDA WA KUPANDISHA NG'OMBE

Mara nyingi dalili za joto huonekana mapema asubuhi au jioni. Ng'ombe wapandishwe masaa 9 hadi 20 tangu kuanza kwa dalili za joto au ng'ombe atakayeonyesha dalili za joto asubuhi ,apandishwe mchana- hadi jioni na atakayeingia jioni, apandishwe kesho yake asubuhi hadi mchana.

6. Kwa maelezo zaidi onana na Wataalam wa upandishaji kutoka Kliniki ya Mifugo ya Halmashauri

# FAHAMU KUHUSU UFUGAJI WA SAMAKI AINA YA SATO

## UTANGULIZI

Ufugaji samaki ni ujuzi unaopewa kipaumbele kwa jamii mbalimbali hapa nchini. Hii ni kwa sababu shughuli hii inaongeza kipato, lishe, na ajira kwa wananchi wanaoshughulika na kazi ya ufugaji. Tunahimiza ufugaji samaki uwiane na kilimo pamoja na wanyama kwa matumizi bora ya maji pamoja na kutunza mazingira. Msisitizo mkubwa ni ufugaji samaki kwa ajili ya biashara na chakula.

Hatua muhimu za kufuata ni:-
Zifuatazo ni sifa za kuchagua eneo linalofaa kwa ufugaji samaki:-

tabia ya samaki bwawani.
Hakikisha bwawa lina upande wenye kina kirefu cha maji (Mita moja na nusu), sehemu hii hutumika kutoa maji bwawani. Pia kuna upande wenye kina kifupi cha maji ( mita moja(1)), sehemu hii huwa na chujio la maji, kawaida ndiyo sehemu inayoingiza maji bwawani.

Kurutubisha maji ya bwawa
Tengeneza sehemu ya kutunzia mbolea (uwigo) ndani ya bwawa kwa kutumia fito na kamba. Rutubisha kwa kutumia samadi ya wanyama mbalimbali wafungwao kama ng'ombe, mbuzi, kondoo, sungura, bata, kuku n.k. pia mboji hutengenezwa kwa kutumia aina mbalimbali za mimea au majani salama. Hakikisha uwingo una mbolea wakati wote.

Kujaza maji bwawa na kupandikiza vifaranga
Kabla ya kujaza maji hakiksha unaweka chujio au wavu kwenye bomba la kuingiza maji ili kuzuia samaki, takataka na mimea isiyotakiwa kuingia Bwawani. Kupandikiza vifaranga kwa kuzingatia idadi inayotakiwa. Bwawa likijaa maji unaweza kupandikiza vifaranga vya samaki, idadi ya samaki utakaopanda iendane na ukubwa wa bwana ili kuhakikisha samaki wanapata, hewa, nafasi na chakula cha kutosha na kukua vizuri. Kiwango kinachoshauriwa ni samaki wanne kwa mita moja ya mraba kwa maana ya majike watatu(3) na dume 1 kwa upandaji wa samaki wenye jinsia tofauti. kwa ufugaji samaki wenye jinsia moja unaweza kupanda samaki 1 hadi10+ kwa mita moja(1) ya mraba iwapo usimamizi utakuwa wa karibu sana "intensive fish farming", katika hali ya usimsmizi wa kawaida "semi intensive

intensive fish farming" ni vizuri ukapanda samaki

4 hadi 5 kwa mita moja(1) ya mraba. Kujua ukubwa wa eneo la bwawa zidisha urefu wa bwawa mara upana(Ur x Up).
Wakati wa kusafirisha vifaranga umbali mrefu vifaranga wanapaswa wavuliwe siku moja kabla na wasilishwe chakula, isipokuwa kama vifaranga watasafirishwa umbali mfupi usiozidi mwendo wa masaa manne(4) hakuna sababu ya kuwavua siku moja kabla.
Vifaranga wasafirisha kwenye maji safi na muda mzuri wa kusafirisha ni asubuhi na jioni ili kupunguza uchovu unaoweza kusababishwa na joto kali.
Mkulima anashauriwa kununua vifaranga bora vya samaki kutoka kwenye vituo vya kuzalisha vifaranga vinavyotambuliwa na serikali na vinavyokidhi viwango vya kitalaam.

Jinsi ya Kulisha samaki
Perege hula chakula cha asili kinachozalishwa kwenye bwawa baada ya kurutubishwa. Pia hupokea chakula cha ziada kilichoandaliwa kwa kuzingatia mchanganyiko wa virutubisho vya lishe kama protini, wanga, madini,vitamini na mafuta.

Maadui wa samaki wanaofugwa kwenye bwawa
Mabwawa ya kufugia samaki yanaingiliwa na maadui wa aina mbalimbali. Baadhi ya maadui hao ni kenge, nyoka, vyura, fisi maji na ndege. Zuia maadui hao kwa kutunza bwawa vizuri. Kwa mfano marekebisho ya kuta na kufyeka majani yanayozunguka bwawa. Pia zipo njia nyingine za kudhibiti maadui hao (rejea mwongozo wa ufugaji wa samaki kwenye mabwawa/ muone mtalaam wa ufugaji samaki aliyekaribu yako).

Mambo muhimu ya kuzingatia unapofuga samaki
Kupunguza idadi ya vifaranga vinapozidi



Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam

Habari Picha

# MADIWANI WA JIJI LA DSM WASHIRIKI NANENANE












Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam

**Habari Picha**

# MADIWANI NA WATUMISHI WA HALMASHAURI WA JIJI LA DSM WALIPOTEMBELEA MAONESHO YA NANENANE KANDA YA MASHARIKI 2023




















Washindi kwa Makundi ambapo Halmashauri ya Jiji la Dar es Salam ilikuwa Mshindi wa kwanza na kupata zawadi ya KOMBE na CHETI.
Washindi kumi wa jumla ambapo Halmashauri ya jiji la Dar es Salaam ilikuwa MSHINDI WA SABA na kwa Halmashauri zote za Mikoa minne Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ilikuwa MSHINDI WA TATU.

Aidha, zawadi kiasi cha fedha shilingi laki tano (500,000/=) kupitia akaunti za benki zilitolewa kwa Mkulima bora NEEMA JOHN MTEI na mfugaji bora WILLY WILLIAM BWEMELO wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ikiambatana na cheti kwa kila mmoja.

HABARI PICHA

# WASHIRIKI WA MAONESHO YA NANENANE 2023 WAKIJIPONGEZA MARA BAADA YA KUKAMILIKA KWA MAONESHO











